https://dspace.org/

# Kati Ya ‘Choo’ Na ‘Msala’ Ni Neno Lipi Tasfida Imetumika Kimatumizi?

**Karama, Mohamed**

**2019-10**
Himaya ya Kiswahili Tol.1 Chapisho la Chama cha Kiswahili Chuwo Kikuu cha Kabianga (CHAKIKA)
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/412

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

**KATI YA ‘CHOO’ NA ‘MSALA’ NI NENO LIPI TASFIDA IMETUMIKA KIMATUMIZI?[1]**

Mohamed Karama, University of Kabianga mkarama@kabianga.ac.ke

**Mukhtasari**

Tasfida ni matumizi ya lugha kwa ustadi unaopunguza makali ya maneno yanayotumiwa. Ikiwa maneno au misemo hiyo ina dalili za kutusi, kukirihi au kuweka maneno mwiko hadharani basi hutumiwa lugha inayoficha sifa hizi mbaya zinazojulikana na jamii. Imejitokeza katika mawanda ya matumizi ya neno ‘choo’ kuwa ni uchafu na hivo wanafunzi wa shule za Msingi na Upili katika mitalaa yao huambiwa wasilitumiye badala yake watumiye ‘msala’ au ‘haja’. Makala haya yameonesha hata hilo neno ‘choo’ piya ni tasfida na lafaa kutumiwa waziwazi katika maongezi ya kawaida. Kufikiya hatuwa hii, tumebainisha matumizi ya maneno ‘choo’, ‘msala’ na ‘haja’ na piya tuliangaziya usuli wa ‘choo’ kiisimu. Uchanganuzi wetu umebaini kuwa neno ‘choo’ latokana na ‘kioo’ lenye maana ya sehemu ya kuoga au kujinadhifisha na hata linapotumiwa kwa maana ya mavi au kinyeshi bado piya ni neno fiche lenye tasfida. Tunahitimisha kuwa kutokana na ‘usafi’ wake, neno ‘choo’ linaweza kutumiwa sawiya na maneno ‘msala’ au ‘haja’ ambayo ni ya mkopo na yenye maana tafauti na kule yalikokopwa.

## Utangulizi

Katika hutuba za Sheikh Abdillahi Nassir zenye anwani “Adabu na Lugha”[2] nimepata kufahamu kuhusu umuhimu wa matumizi ya lugha na kutunga adabu wakati wa kuzungumza. Katika hutuba hizo mumeelezwa kuhusu lugha na namna Waswahili wanavotunga mila na dasturi zao wakati wanapozungumza baina ya wazee na kati ya watoto na wazee. Sheikh amesisitiza utumiyaji wa lugha ‘kifasaha’ kwa maana ya kuilekeza lugha katika mkonro wa adabu zake. Si ajabu kwamba katika anwani ya hutuba hizo neno ‘adabu’ nrilo lililokuja mwanzo.

Katika maskuli ya humu nchini Kenya, suala hili la matumizi ya lugha na kutunga adabu za mazungumzo piya ladhihirika. Katika mitalaa ya kufunziya Kiswahili maskuli, wanafunzi huelezewa maana ya maneno na kwa nini yakatumika kwa ndiya hiyo. Piya, hupawa istilahi ya matumizi ya aina hiyo ya lugha inayoitwa tasfida. Kulingana na Njogu

---

# Makala haya yalichapishwa katika *Himaya ya Kiswahili* Tol.1 Chapisho la Chama cha Kiswahili Chuwo Kikuu cha Kabianga (CHAKIKA), Oktoba, 2019, uk.6-8.

[1] Nawashukuru walimu wangu wote walonisaidiya kwa fikra ili nitowe maoni yangu. Myongoni mwao Ust. Mau, Ust. Mohammed Hassan Mpate, Ust. Ahmed Hussein Jitu Kali na wanafunzi wangu wote tuliyojadiliyana kuhusu makala haya.

[2] Nililetewa hutuba hizi na Prof. Abdilatif Abdalla kutoka maktaba yake binafsi.

na Chimerah (1999:33) wanasema, "tasfida ni kutumiya lugha safi (iliyochujwa) ili maneno machafu au yanayokirihi yasitumike. Kwa mfano, badala ya kusema "fulani ana mimba" unasema "fulani ni mja mzito". Usemi wa pili ni tasfida. Piya, badala ya kusema "fulani amekufa" unasema "fulani ameaga duniya" au "amefariki (duniya)". *Hii nriyo adabu ya lugha* (msisitizo ni wangu)." Kwa mnasaba huu wa kutunga adabu wakati wa kutumiya lugha katika jamii au kunri la watu mahususi, nripo nilipokuja kuwaza kuhusu matumizi ya 'choo' katika lugha ya watu wa kawaida Uswahilini. Maskulini na katika maongezi ya kirasmi inaambiwa kwamba kutumiya neno 'choo' ni kutotunga tasfida. Kwa maana nyengine yaweza kutukuliwa kuwa mtumiyaji wa neno 'choo' haelewi adabu, mila wala dasturi za lugha ya Kiswahili.

Lengo la makala haya ni kutaka kugeuza fikra hii kwamba 'choo' ni neno chafu na halifai kutumiwa kama wanavotwambiya walimu wetu maskulini, na piya, kwa kutojuwa, hata Waswahili wenyewe wamekuja kukubali hivo. Kufikiliya shabaha hii tutabainisha matumizi mbali mbali ya neno 'choo' katika lugha ya Waswahili; tutafafanuwa usuli wa neno 'choo' na 'msala'; na katika hitimisho letu tutabainisha uwafiki wa matumizi ya neno 'choo' katika maongezi ya kawaida kwa kuwa limetunga tasfida. Uchunguzi wetu utakuwa wa kisinkroniya. Yaani, tutachambuwa kiisimu miunri inayojenga neno 'choo' bila ya kuangaliya historiya au mabadiliko ya maana ya neno lenyewe katika mpito wa wakati.

## Maana na matumizi ya maneno 'choo', 'msala'

Kulingana na Krapf (1822:40) neno 'choo' lina maana ya 'mahali pa kunyiya', na 'msala' ni 'jamvi au mkeka wa kuswaliya' (245). Naye Sacleux (1939:149) anaeleza kuwa 'choo' ni mahali pa faragha; mahali pa kunyiya; chumba. 'Msala' ni mkeka duaradufu unaotumiwa na Waislamu kuswaliya (593). Madan (1903:45) anafafanuwa 'choo' kuwa 'sehemu yenye linri mviringo na mawe mawili pembezoni. Kawaida huunganishwa na maliwato kwenye majumba makubwa'. Madan anasema kwamba 'msala' ni (1) mkeka duaradufu unaotumiwa kuswaliya (2) ni mahali faragha, maliwato, chumba (1903:246). Kamusi ya Wiktionary inaeleza 'choo' kuwa (1) ni chumba au mahali penye kifaa cha kuenra haja. Kamusi inatowa kisawe cha 'choo' kuwa ni msala: sehemu ya kwenra haja yaani *toilet* kwa Kiingereza. Kulingana na *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* ya TUKI (2006) inatafsiri *toilet* kuwa 'choo, msala' na *lavatory*, *loo*, *restroom*, kuwa 'msala'. Makamusi ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013:78) na *Kamusi ya Karne 21* (2011:70) maelezo yao kuhusu 'choo' ni mahali pa kunyiya piya ni kinyeshi kitokacho kutoka tupu ya nyuma. Msala ni mkeka wa kuswaliya na piya ina maana ya choo (sehemu ya kunyiya). Kulingana na vijelezi hivi tulivonukuu makamusini tunaona kwamba 'choo' ni mahali maalumu pa kunya au mahali pa kukojowa. Vilevile 'msala' ina maana ya sehemu maalumu ya kuogeya, kunyiya na piya ina maana ya mkeka au jamvi la kuswaliya.

Kimaongezi katika jamii ya Waswahili watu husema 'kwenra chooni' kwa maana ya mahali pa kunya. Au, kuelezeya mavi/kinyesi/chudhi au mkojo watu husema 'choo kikubwa' na 'choo kidogo' mtawaliya. Piya watu husema "mtoto/mgonjwa amepata au ameenra choo leo" kwa maana ya ametokwa na mavi. Katika maelezo mengine niliyoyapata kuhusu maana ya 'choo' ni lile jengo, sehemu au mahali penye linri na

maliwato (sehemu ya kunyiya na kuogeya mtawaliya) nrani yake. 'Choo' piya ina maana ya kifaa kinachotumiwa kupokeya mavi au mkojo, yaani 'choo cha linri', 'choo cha sahani' au 'choo cha kinu'. Katika matumizi mengine ya kitasfida kuhusu 'choo' kwa maana ya mavi au mikojo ni 'haja'. Kwa hivo, watu husema 'nenra haja' (kitenro cha kunya/kukojowa) au 'haja kubwa/nrogo' (mavi/mkojo). Kulingana na Sheikh Abdillahi 'haja' (nikimnukuu kutoka kwenye kanra hizo za hutuba zake na matumizi katika *Kamusi ya Shule za Msingi* ambamo yeye ni mmoja wa waandishi) nriyo matumizi muwafaka zaidi yenye kutunga adabu na dasturi za mazungumzo ya Waswahili. Kulingana na walimu wa maskuli (wakati wa majadiliyano na wanafunzi wangu) wanasema na kushikiliya kuwa 'msala' ni muwafaka zaidi kutumiya kwa sababu ni 'safi' kutumiya kuliko 'choo'.

**Usuli wa Kiisimu wa neno 'choo'**

Choo ni Nomino Kawaida iliyoko katika ngeli ya KI-VI. Katika uchache ni 'choo' na wingi wake ni 'vyoo'. Kimofolojiya ni mofimu yenye mofu tatu {ki-} + {-o } + {o}. Kutokana na mifanyiko ya kimofofonolijiya fonimu /ch/ imepatikana baada ya sauti ya /ki-/ kukaakaaishwa kwa sababu ya kukutana na irabu katika mofimu {-oo}.

/ki-/ + /-oo/ ⟶ /kyoo/ ⟶ /choo/

Mofimu /ki-/ inapokutana na mofimu ya irabu /-oo/ huleta /kyoo/. Lakini kwa sababu ya ikitisadi na urahisi wa kutamka /ky/ inayotamkwa kwenye kaakaa laini hugeuzwa na kufanywa itamkwe /ch-/ kwenye kaakaa gumu. Nripo sana tukapata /choo/. Mifano ya mfanyiko huu ni kama /changu/ ambayo imetokana na /ki- + -angu/.

Baada ya kuona kwamba 'choo' ni mshikamano wa mofimu tatu {ki-} (kiambishi cha ngeli ya 7 KI) na {-o-} ambayo ni mzizi wa kitenzi na mofimu {-o} ya mwisho ni kiambishi tamati cha kuashiriya kile kifaa kinachofanya kitendo na piya huonesha matokeo ya mwisho ya kitendo hicho. Kulingana na Mohamed (2001:32) viambishi KI-, au piya U-, M-, MA-, na NY- huambishwa mwanzoni yenye maana ya kifaa kinachofanya kitendo hicho.

Funika – (ki)funiko
Ziba – kizibo
Vuka – kivuko
Lisha – malisho
Unda – nyundo
Shona – mshono
Sema – msemo.

Kutokana na mifano hiyo tutaona kwamba choo ilitokana na kioo ambapo humaanisha kifaa (mahali) kinachotumiwa kwa oa.

Ushahidi wa maana ya {oa} kuwa ni kuoga tunapata katika shairi la Muyaka katika (Abdulaziz, 1979:182). Muyaka anasema:

4. Oa, maji ya kisima, yatengenywe na mvuwa
Oa, ukijitezama, kioo ukichanguwa
Oa, mwanamke tama, mtukufu wa sitawa
Oa! Sizi ndizi ndowa. aso kuoa ni yupi?

Katika mshororo wa kwanza Muyaka anamwambiya mhusika wake aoge kwa maji ya kisima yaliyotanganywa na ya mvuwa. Mshororo wa pili anamwambiya ajiangaliye kwenye kioo na mshororo wa tatu anamwambiya aowe mke mwenye utukufu kama yeye. Abdulaziz katika tanbihi ya shairi hili katika ukurasa wa 183 anasema hili ni shairi la kihomonimi ambapo neno 'Oa' lina maana ya kuoga, kuangaliya, kufunga nrowa. Kutokana na ubeti huu, tunatukuwa kwamba choo ni kifaa au ni sehemu ya kuoga yenye maana nasibishi ya kujinadhifisha kwa maana ya mshororo wa kwanza.

Uchunguzi wetu kuhusu neno 'msala' au 'haja' unatuonesha kuwa, kwanza, ni maneno ya Kiarabu na piya yana maana tafauti katika Kiarabu si kama yalivo katika Kiswahili. Kwa Kiarabu, 'msala' ina maana ya 'mahali pa kuswali' kulingana na *A Dictionary of Islamic Terms* (h.t:103) na 'haja' katika kamusi ya *Al Mawrid Arabic-English* (1995:442) ina maana ya 'utashi wa kitu'. Hatuwezi kukataa maana inayotumika katika Kiswahili hivi sasa kwa sababu maneno hayo (msala na haja) tayari yashaingiya na yashasakini hata yamekubalika kwa maana hizo tafauti na kule yanakotoka. Kwa hivo, ni sahihi tukisema kwamba choo ni msala au ni mahali pa haja.

## Mjadala wa Matokeo

Kutokana na ushahidi wa kiisimu na wa shairi la K19 kwamba 'choo' ni chombo (sehemu) na ni kuoga basi hata choo ni tasfida na halina chembe ya uchafu. Hivo, laweza kutumika kwa maana moja na 'msala' na 'haja'. Pili, neno haja ni neno la kijumla lenye maana ya utashi wowote ikiwa ni kunya au kutaka kumuona mtu ofisini. Choo lina maana mahsusi na lahusishwa na kuonrowa uchafu mwilini na limefinika uchafu huwo bila ya kuutaja waziwazi. Tatu, kulingana na msailiwa mmoja alinambiya kwamba neno 'msala' lina athari za kiutakatifu kama tulivoona hapo awali kwamba lamaanisha mahali pa kuswali. Piya msala limesaki kwenye maana moja tu ya mahali pa kuoga au kunya ilhali choo lina maana nyingi: mavi, kuoga, sehemu ya kufanya mahitajiyo hayo ya kibinadamu, na kifaa cha kupokeya uchafu huwo.

Kimatumizi kwenye lugha ya kirasmi na kikawaida, Waswahili wa Mkowa wa Pwani Kenya mpaka leo wanasema 'nenra chooni' kwa kutaka kunya, kukojowa, au kuoga. Pili, katika masimulizi ya kawaida hatukuwasikiya wakisema, "leo mtoto/mgonjwa amepata mavi/kinyesi" kwa kutumiya nahau ya 'kwenra choo(ni)', 'choo kikubwa' au 'choo kidogo'. Je, watumiyaji wa 'msala' kwa maana mahususi ya mahali pa kunya na wala si mahali faragha haionekani kwamba nrugu wengine Uswahilini 'wanaudhika' kwa kulinganishwa mahali pa swala (maombi kwa Mungu) na mahali pa kunyiya mavi?

## Hitimisho

Katika makala haya tumeweza kuona kwamba neno ‘choo’, ‘haja’, na ‘msala’ yana maana ya sehemu ya kuoga au kwenra kunya na hutumika kwa kubadilishana. Vijelezi kutokana na makamusi tuliyonukuu na matumizi maskuli huku Kenya yanasadikisha maelezo hayo. Ushahidi wa kiisimu unaonesha kwamba ‘choo’ asili yake ni ‘kioo’ yenye maana ya chombo kinachotumika kwa kujinadhifisha. Ushahidi wa shairi la Muyaka nriwo unaotuhakikishiya kuwa oa ni kuoga. Kwa hivo, kwa kutumiya ‘choo’ msemaji huwa tayari ameshatumiya tasfida na ametunga adabu ya lugha kwa kuita mavi (uchafu) choo iliyo na athari za usafi. Makala haya yanadhibiti lengo lake kwamba neno ‘choo’ ni muwafaka kutumiwa katika muktadha wa kirasmi na piya katika maongezi ya kijamii kwa sababu halina chembe za maana ya uchafu na limetunga adabu za lugha ya Kiswahili. Makala yanaamini kuwa utafiti mwengine mpana ufanywe kuhusu maneno ambayo yanadhaniwa kuwa ‘machafu’ na ilhali maneno hayo ni muwafaka kutumiwa katika maongezi rasmi au ya kikawaida. Kwa mfano, matumizi ya neno ‘matako’? Je, mbali ya kigezo cha tasfida, kuna uwezekano wa kudhibiti mabadiliko ya maana za maneno ili yasipotoshwe au yasipotoshe jamii? Ni utafiti wataka fanywa huwo.

## Marejeleo


Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th century popular poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Alkhuli, M. A. (h.t). *A dictionary of Islamic terms*. pdf

Baalbaki, R. (1995). *Al Mawrid*: *A modern Arabic-English dictionary*. Beirut: Dar ilm lil Malayin.

Choo. (2011). *Kamusi ya Karne 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. London: Trubner & Co.

Madan, A. C. (1903). *A dictionary of Swahili-English*. Oxford: Clarendon Press.

Mohamed, M. A. (2001). *Modern Swahili grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Nassir, S. A. (h.t). *Adabu na lugha* [CD]. Mambasa. Abdilatif Abdalla (hazina binafsi).

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Sacleux, C. S. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Paris: Institut d' Ethnologie.

TUKI, (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Daresalaam: TUKI.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.